Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

SEHEMU E (ALAMA 45) FASIHI KWA UJUMLA

Jibu maswali matatu kutoka sehemu hii. Swali la 15 ni lazima.

11. "Sifa muhimu mojawapo ya methali ni kujenga picha au taswira ambazo huchotwa katika mazingira yanayoizunguka jamii. Thibitisha hoja hii kwa kutumia methali tano (5)
12. Waandishi wa tamthiliya wameibua na kubuni jina la kitabu ambalo linasadifu yaliyomo ndani ya kazi zao. Thibitisha kauli hii kwa hoja tatu (3) kutoka kila tamthiliya kati ya mbili ulizosoma.
13. "Ukinzani ni jambo lisiloepukika ndani ya jamii" kwa kutumia hoja tatu (3) kutoka kila riwaya kati ya mbili ulizosoma. Jadili kauli hii.
14. Taswira ni kipengele muhimu katika kazi ya fasihi kwani hujenga picha na kumfikisha msomaji wa kazi ya fasihi. Kwa kutoa hoja tatu kutoka katika kila diwani kati ya mbili ulizosoma. Jadili kauli hiyo.
15. Umeteuliwa kushiriki katika uandishi wa ngonjera kwenye shindano la wanafunzi wa Afrika ya Mashariki. Tunga ngonjera yenye beti nne (4) kuhusu madhara ya simu kwa wanafunzi shuleni.

ORODHA YA VITABU TEULE;

USHAIRI

Wasakatonge *M.S. Khatibu (DUP)*
Malenga Wapya *TAKILUKI (DUP)*
Mashairi ya Cheka Cheka *T.A. Mvungi (EP & D.L.T.D)*

RIWAYA

Takadini *Ben Hanson (MBS)*
Watoto wa Mama N'tilie *E. Mbogo (H.P)*
Joka la Mdimu *A.J. Safari)H.P)*

TAMTHILIYA

Orodha *Steve Reynolds (MA)*
Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe *E. Semzaba (ESC)*
Kilio Chetu *Medical Aid Foundation (TPH)*

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE REGINAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

SIKONGE SECONARY SCHOOLS EXAMINATION SYNDICATE (SISSES)

FORM FOUR MOCK EXAMINATIONS - SEPTEMBER, 2018

MSIMBO: 021 KISWAHILI

MUDA: SAA 3:00 JUMATANO: 29/08/2018 (Mchana)

MAELEKEZO:

1. Mtihani huu una sehemu tano (5) A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, B, D swali moja kutoka sehemu C na maswali matatu (3) kutoka sehemu E swali la 15 ni la lazima.
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na kila swali.
4. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa karatasi za kujibia.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU.			
NAMBA	**SWALI LILILOFANYIKA**	**ALAMA**	**JINA LA MSAHIHISHAJI**
1			
2			
3			
4			
5			
6			
7			
8			
9			
10			
11			
12			
13			
14			
15			
JUMLA			

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

SEHEMU A (ALAMA 10) UFAHAMU

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika majibu sahihi.

Watu wengine wanasema “Elimu ni Bahari” Bila shaka wanasema kweli kwa sababu idadi ya elimu ni nyingi sana, nazo hazihesabiki. Hebu fikiria kidogo juu ya mwili wa mwanadamu, roho yake, sehemu mbalimbali za mwili wake kama vile macho, masikio, mifupa, moyo, miguu na kadhalika. Fikiria tena elimu inayohusu wanyama mbalimbali na tabia zao, nyota na vitu vilivyomo angani, dini za kila aina, dawa za kila aina, utawala wa nchi kujenga nyumba, lugha mbalimbali, desturi za watu na mambo mengine mengi kabisa. Lakini kila mtu anaweza kusomea habari za elimu hizo akipenda kwa sababu habari hizo zimetungwa na watu wenye maarifa nazo zinapatikana katika vitabu vilivyopigwa chapa.

Binadamu hawana maisha marefu. Kweli watu wengine hujaliwa kuishi kwa muda mrefu mpaka kufikia umri wa miaka themanini au zaidi. Hebu tujaribu kufikiria tena kama binadamu wasingeweza kuandika wala kutunga vitabu na kuvipiga chapa. Tuchukue mtu anayependa kufikiri sana na kutafuta habari za dawa naye akapata kujua habari za dawa nyingi sana. Kama hawezi kuandika, itambidi ayazingatie maarifa yake kwa njia ya kukumbuka tu. Mtaalamu huyu itampasa kuwaambia wanafunzi wake habari za dawa alizovumbua nao vilevile kama hawajui kuandika watalazimika kuzikumbuka kwa akili tu.

Basi kwa bahati mbaya yule mwenye maarifa akipatikana na maradhi na kupitiwa na faradhi, pengine wanafunzi wake watakumbuka maarifa mengine aliyowaambia. Lakini yale mengine ambayo hakuwaambia atakufa nayo. Wanafunzi itawabidi kufanya bidii wakitaka kuvumbua maarifa yale yaliyopotea. Basi elimu ya mtindo huu haiendelei sana kwa sababu kila mara mtaalamu wa namna hii anapokufa hufa na maarifa mengi aliyovumbua na kila kizazi kitaanza upya kuvumbua yale yale badala ya kuvumbua mapya ili kuendeleza elimu hiyo.

Tatizo la namna hii halitokei katika jumuiya ya binadamu wajuao kusoma na kuandika. Iwapo mtaalamu akivumbua maarifa ya jambo lolote huandika habari zake, watu watakapokuja baada yake watakuwa na kumbukumbu nalo kwa kuvisoma vitabu alivyotunga, na pia wataweza kuyaendeleza maarifa hayo na kuvumbua mengine mapya.

MASWALI:

(i) Mwandishi analinganisha Elimu na Bahari, ni kwanini?

(ii) Mtu mwenye maarifa anaweza kupitiwa na faradhi. Neno faradhi lina maana gani?

(iii) Hapo zamani hapakuwa na maandiko, nini kilifanyika kwa wanafunzi wapya?

(iv) Kuna hatari gani ikiwa watu watakuwa na maarifa lakini hawajui kusoma wala kuandika?

(v) Ni jambo gani muhimu kwa watu wajuao kusoma na kuandika?

2. Kwa kuzingatia habari uliyoisoma fupisha aya ya kwanza kwa sentensi tatu tu.

SEHEMU B (ALAMA 25) SARUFI

3. (a) Nini maana ya viambishi awali?
   (b) Onesha viambishi awali vinavyobadili neno “Lima” kwa kupigia mstari kiambishi kinachodokeza: (i) Njeo (ii) Nafsi (iii) Urejeshi (iv) Ukanushi
4. Yapo mambo mbalimbali yanayoweza kusababisha uvulivuli katika lugha. Kwa kutoa mifano anuai taja mambo matano.
5. “ Uchanganuzi wa sentensi hufanyika hatua kwa hatua” Ukitumia hatua hizo kwa kutumia mkabala wa kisasa changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya mishale.
   (a) Baba na mama wanalima (b) Mtoto alilia sana alipochapwa.
6. Bainisha njia zilizotumika katika uundaji wa maneno yafuatayo:
   (i) Kizunguzungu (ii) Chamcha (iii) Malapa (iv) Korokoroni (v) Ufunguo
7. Kitenzi kishirikishi (t) hudhihirisha kwa mambo mbalimbali kwa kutumia mifano kuntu taja mambo matano ya kitenzi kishirikishi.

SEHEMU C (ALAMA 10) UANDISHI

8. Kwa kutumia majina ya kubuni na mada ya kubuni andika kumbukumbu za kikao.
9. (a) Eleza kwa ufupi tofauti iliyopo baina ya hotuba na risala.
   (b) Wewe ni diwani katika kata ya Shighatini. Umeombwa kuwa Mgeni rasmi katika mahafali ya kuhitimu kidato cha nne katika shule ya Sekondari Kilobeni. Andika hotuba ya maneno kati ya 150 – 200 utakayotoa katika sherehe hiyo.

SEHEMU D (ALAMA 10) MAENDELEO YA KISWAHILI

10. Baada ya Kiswahili kuteuliwa kuwa lugha ya Taifa vyombo mbalimbali viliundwa kwa lengo la kukuza na kueneza Kiswahili. Thibitisha dai hili kwa kutumia asasi nne (4)

Search ⇢ www.africona.net